



HALMASHAURI YA WILAYA YA KALIUA

S.L. P 83, KALIUA, Simu Na: 0736 204 192,
Nukushi: 0732 988 451, Barua pepe: ded@kaliuadc.go.tz,
Tovuti: www.kaliuadc.go.tz

KDC/M.2/VOL II/0056/51

19/07/2018

TANGAZO LA NAFASI YA KAZI YA DEREVA - NAFASI 2.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua anawatangazia Wananchi wote wenye sifa, nafasi ya kazi ya Udereva kama ifuatavyo;-

DEREVA DARAJA LA II (DRIVERS II) NAFASI - 2

A. SIFA ZA KUINGILIA MOJA KWA MOJA

1. Kuajiriwa mwenye cheti cha mtihani wa Kidato cha nne (iv), mwenye leseni daraja "E" au C1 ya uendeshaji magari ambayo amefanyia kazi kwa muda usiopungua mwaka mmoja bila kusababisha ajali. Awe amehudhuria mafunzo ya msingi ya uendeshaji magari(Basic Driving Course) yanayotolewa na Chuo cha mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA) au chuo kingine kinachotambuliwa na Serikali. Waombaji wenye cheti cha majaribio ya Ufundi Draja la II watafikiriwa kwanza.

2. KAZI ZA KUFANYA:

1. Kukagua gari kabla na baada ya safari ili kubaini hali ya usalama wa gari
2. Kuhakikisha gari na vyombo vyake viko katika hali nzuri wakati wote, na kufanya uchunguzi wa gari kabla na baada ya safari ilikugundua ubovu unaohitaji matengenezo.
3. Kufanya matengenezo madogo madogo katika gari
4. Kutunza na kuandika daftari la safari " Log-book" kwa 0 safari zote.

B. NGAZI YA MSHAHARA

Mshahara ni kwa mujibu wa viwango vya mishahara Serikalini yaani TGS B

C. MASHARTI YA JUMLA

- i. Mwombaji awe raia wa Tanzania
- ii. Mwombaji awe na umri usiozidi miaka 45 na awe hajawahi kupatikana na kosa la jinai au kufungwa jela.
- iii. Maombi yote yaambatanishwe na maelezo binafsi yanayojitosheleza (Detailed cv)
- iv. Maombi yote yaambatanishwe na nakala za vyeti vya taaluma, vyeti vya elimu (IV au VI), cheti cha kuzaliwa na picha mbili za rangi za hivi karibuni (passport size) Ziandikwe jina la mwombaji nyuma.
- v. Testimonials Provisional results "Statement of results" hati ya matokeo ya kidato cha nne na sita
- vi. Waombaji wote waliostaafishwa au kuondolewa katika Utumishi wa Umma hawaruhusiwi kuomba isipokuwa kwa kibali cha Katibu Mkuu Kiongozi.
- vii. Waombaji waliosoma nje ya Tanzania wahakikishe vyeti vyao vimehakikiwa na mamlaka husika
- viii. Waombaji watakaowasilisha taarifa na sifa za kughushi wahusika watachukuliwa hatua za kisheria

Maombi yatumwe kwa:-
MKURUGENZI MTENDAJI,
HALMASHAURI YA WILAYA,
S. L. P. 83,

KALIUA.

Tarehe ya mwisho ya kupokea maombi ni tarehe 01/08/2018 saa 9.30 mchana.


Edwin Mashala

KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI (W)
HALMASHAURI YA WILAYA
KALIUA

KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA
KALIUA

Barua zote zitumwe kwa Mkurugenzi Mtendaji Wilaya)